TANGAZO LA SERIKALI NA. 26 la tarehe 17/02/2017

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

## SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE, 2017

### SEHEMU YA KWANZA

### UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo;

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

Sura 206

"Eneo la Hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, maeneo ya Vyanzo vya Maji, Hifadhi ya Misitu, Miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mlele;

"Kiwanda" maana yake ni Jengo au majengo ambapo vitu vinatengenezwa;

"Kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata, kung'oa miti au visiki;

"Mabwawa" maana yake ni sehemu yoyote yenye mkusanyiko wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

"Machungio" maana yake ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kulishia mifugo.

Maji" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kuwa ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito, vijito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji yaliyoko chini ya ardhi, maji yaliyoko katika makondo;

Na. 20 ya Mwaka 2004

"Mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kuwa ni kitu cho chote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuto, nyuzi za wanyama, mimea au kitu chochote chenye uhai au kisicho kuwa na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la msitu;

Na. 20 ya Mwaka 2004

"Mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kuwa ni maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia ya nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali ya kibiolojia za wanyama na mimea, raslimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"Mti" maana yake ni mti uliopandwa na miti asili ikiwa ni pamoja na mianzi, vichaka, mapori, maotea ya msituni ya umri mbalimbali na aina tofauti;

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji wa mifugo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumju ya Mkurugenzi;

"Misitu maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi amabayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"Taka" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kuwa ni kitu chochote kimiminika, kigumu, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira ambayo inajumuisha taka;

Na.14 ya mwaka 2002

"Taka ngumu" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kuwa ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi, plastiki au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini,mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu;

Na. 20 ya Mwaka 2004

"Uchafuzi wa mazingira" maana yake ni uchafuaji wa mazingira kwa namna yoyote ile unaotokana na utupaji wa kitu chochote baada ya kukitumia au uwekaji wa kitu chochote katika eneo ambalo hakikustahili kuwepo au mwingiliano wa sauti za juu kutoka kwa watu au

vyombo mbalimbali ambavyo husababisha usumbufu wa kimazingira, hewa chafu, maji na vitu vyovyote vile ambavo husababisha uchafuzi katika hali yoyote ile;

"Udongo maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kuwa ni pamoja na ardhi, mchanga, mwamba,tope, madini, uoto na viumbe waishio humo na vyote vitokanavyo kama vile vumbi;

”Vitu hatari” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Kuwa kemikali yo yote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira.

“Uharibifu” maana yake ni mabadiliko ya moja kwa moja ya rasilimali za kimaumbile, hali ya joto, kemikali, kibaolojia ambazo ni kikwazo cha sehemu ya mazingira na hivyo kuleta madhara kwa matumizi yenye manufaa, au kusababisha hali ambayo ni hatari kwa jamii kiafya, kiusalama au ustawi wa binadamu na mazingira;

## SEHEMU YA PILI
### MASHARTI YA UFUGAJI

Wajibu wa mfugaji

4. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi;

(a) Atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoamriwa na Halmashauri;

(b) Atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;

(c) Atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia (stock routes) zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(d) Atatakiwa kuwa na Kadi ya Mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(e) Atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri;

(f) Atatakiwa kupeleka Mifugo yake katika Vituo

vya Chanjo kama itakavyoamuriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;

(g) Atatakiwa kuchangia gharama za ukarabati wa Majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;

(h) Atatakiwa kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;

(i) Atatakiwa kuweka alama kwenye mifugo yake (Branding, ear tags) na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la Ngozi;

(j) Atatakiwa kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyo hitajiwa na Halmashauri;

(k) Atatakiwa kutokata miti kwa lengo la kufukuza Mbung'o.

Masharti ya mfugaji

5. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote:-

(a) Kuchunga, kulisha, au kunywesha maji Mifugo katika maeneno ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;

(b) Kusafirisha Mifugo kwa kuiswaga Barabarani;

(c) Kusafirisha au kuhamisha Mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila Kibali cha Afisa Kilimo na Mifugo;

(d) Kuuza au kununua Mifugo katika maeneo ambayo siyo ya mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;

(e) Kufuga Mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri;

(f) Kupitisha mifugo yake katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha Mifugo.

Kuthibiti mifugo inayozurura ovyo

6(1) Halmashauri itakamata Mifugo au Mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia Mifugo.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini kama itakavyopangwa na Halmashauri na baada ya kulipia gharama hizo Mfugaji atarudishiwa Mifugo yake.

(3) Endapo mwenye Mifugo au Mfugo hatakokea ndani ya siku saba tangu kukamatwa kwa Mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada Mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo kufanyika, Mkurugenzi atakata fedha ya faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye Mifugo na kama hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri.

(5) Endapo mwenye Mifugo au Mfugo atakuwa na sababu za msingi za kutofika ndani ya siku kumi na nne (14) tangu kufanyika kwa mnada Halmashauri itarudisha fedha zake.

(6) Endapo kutatokea uharibifu kwa Mifugo au Mfugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama uharibifu huo umesababishwa na uzembe wa Halmashauri, Halmashauri itawajibika kwa uzembe huo.

Ukaguzi wa mifugo

7(1) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo na Mifugo, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji, na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika Nyumba au jengo lo lote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya Mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.

(2) Mtu yeyote atakaye wazuia Maafisa Waidhiniwa katika Kifungu cha 7(1) kutekeleza wajibu wao chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

8(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga Maeneo maalumu kwa ajili ya shughuli za Malisho kwa kuzingatia idadi ya Mifugo ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Halmashauri itatenga njia maalumu ya kupitisha Mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za Mifugo ikiwa ni pamoja na kusajiri mifugo yote na kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za ufugaji

9(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria

ye yote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mifugo au mfugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinjia mnyama mahali pengine popote.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

## SEHEMU YA TATU
### KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

Taratibu za kilimo

10(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za Kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri.

(2) Itakuwa halali kwa Afisa kilimo kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Masharti kwa mkulima

11(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia Ushauri wa Afisa Kilimo.

(2) Ni marufuku kwa mtu ye yote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kusafisha Shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha mandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimizi kilimo cha mzunguko (crops

rotation).

Uhifadhi wa uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake ya awali.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13. Ni marufuku kwa watu ye yote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kandokando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Halmashauri.

Marufuku

14. Ni marufuku kwa mtu ye yote kujenga Nyumba au Jengo lolote katika eneo la hifadhi.

## SEHEMU YA NNE
### HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

15 Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

Kulinda eneo la hifadhi

16(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchanga mifugo katika katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika Vyanzo vya Maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Msitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha Maji isipokuwa Halmashauri.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

17(1) Ni marufuru kwa mtu yeyote, Kiwanda, Taasisi, Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemichemi au sehemu yo yote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya

matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe cho chote hai.

## SEHEMU YA TANO
### HIFADHI YA MISITU

Kuchoma au kusababisha moto

18(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, Kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, na kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Kibali cha kuchoma moto

19 Mtu ye yote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma moto na ataweka njia za kuzuia moto

Ukataji miti

20(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi husika.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu

ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu amabao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanao vuna miti ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalumu lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Wajibu wa kupanda miti

21 Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika:-

(a)Kupanda na kutunza miti katika eneo lake;
(b)Kupanda na kutunza miti katika makazi yake;
(c)Kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki

Wajibu wa vijiji

22 Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila Kijiji;

(a) Kitawajibika kutenga eneo la Hifadhi ya Msitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadaye;
(b) Kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la kijiji;
(c) Kitahakikisha kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake;
(d) Mtu yeyote atakayetaka kukata miti au mti kwa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli zinginezo, itambidi apate kibali cha maandishi kutoka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji na Kibali cha Afisa Maliasili wa Wilaya au wasaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri;
(e) kila shule au taasisi nyingine itapaswa kupanda miti kukinga upepo kuzunguka majengo yake na kuwa na shamba lilisopungua miti hekta mbili;
(f) Kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na Vyanzo vingine vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;

(g) Kila Mwenyekiti wa Kitongoji, Mtendaji wa kijiji,au Mkuu wa Taasisi yoyote atahakikisha kuwa Kijiji au Taasisi ina msitu wa hifadhi ya miti ya kupandwa au ya asili iliyotengwa kwa

madhumuni ya kuhifadhi Ardhi, Mazingira na matumizi ya baadaye.

## SEHEMU YA SITA
### TAKA NGUMU NA LAINI

Utupaji wa taka ngumu na laini

23(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia katika kingo za maziwa, mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa viwanda

24 Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yo yote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

## SEHEMU YA SABA
### MAKOSA NA ADHABU

Makosa yanayohusu mifugo

25 Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa ikiwa:-

(a) ataingiza Mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(b) atasafirisha Mifugo bila kuwa na Kibali;

(c) atalisha Mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(d) atafuga Mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;

(e) atavua Samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo.

Makosa yanayohusu kilimo

26 Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Kilimo, kuchimba Mchanga, Kokoto, Madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu Ardhi

27 Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kuhifadhi Ardhi atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu Maji

28(1) Mtu yeyote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu ye yote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yo yote kwa namna yoyote ambayo itaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.

Makosa ya kuharibu misitu

29 Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa ikiwa:-

(a) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali au;

(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto au;

(c) atavuna Mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali au;

(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali au;

(e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na visiki kwenye misitu bila kibali;

(f) atachoma au kusababisha moto katika msitu bila kibali;

(g) atachunga mifugo kwenye eneo lo lote lililopandwa miti au iliyohifadhiwa kama bustani ya miti;

(h) atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;

(i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, mlima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zilizohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngumu na laini

30 Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa na Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yo yote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu taka za majimaji

31 Mtu yoyote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu viwanda

32 Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka, mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa.

Adhabu

33 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imebandikwa katika Sheria hizi Ndogo kutokana na Azimio la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kilichoketi tarehe 17 mwezi 07 mwaka 2015 na lakiri imebandikwa mbele ya:-

GODWIN L. BENNE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

DUES J. BUNDALA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*